

Mambo Yote Kuhusu Punguzo la Gharama Shirikishi

# Gharama Nafuu Zinaweza Pesa Mifukoni Mwako



## GHARAMA SHIRIKISHI NI NINI?

Punguzo la gharama shirikishi linapunguza gharama unazolipia wewe za bima yako ya afya (makato, malipo shirikishi na bima shirikishi). Halipunguzi malipo yako ya bima. Unaweza kuipata tu kupitia *Washington Healthplanfinder*.

## NAWEZAJE KUPATA PUNGUZO LA GHARAMA SHIRIKISHI?

Unapata punguzo la gharama shirikishi kulingana na kipato chako. Kipato chako kikiwa kidogo zaidi, vivyo hivyo punguzo lako. Jiunge na kifurushi cha Fedha kupata punguzo la gharama shirikishi.

## NINI FAIDA YA PUNGUZO LA GHARAMA SHIRIKISHI?

**Linapunguza makato yako.** Ukiwa na makato ya chini, bima yako ya afya itaanza kushiriki gharama muda mfupi zaidi.

**Linapunguza malipo shirikishi na bima shirikishi.** Unalipa malipo na bima shirikishi ukipokea huduma inayolipiwa bima. Punguzo la gharama shirikishi linapunguza kiasi cha malipo haya.

**Linapunguza kiasi cha juu unacholipia kutoka mfukoni.** Kiasi cha juu unacholipia kutoka mfukoni kipunguza kile unacholipia kwa huduma ya afya kwa mwaka. Huduma zinazolipiwa bima hazina kiasi unacholipia kutoka mfukoni ukifikia ukomo huu.

## PATA USAIDIZI UKIUHITAJI

Wahudumu wetu wa Kituo cha Usaidizi kwa Wateja wanaweza kujibu maswali na kukuunganisha na mtaalamu katika eneo lako.



Tupigie  
**1-855-923-4633**



Tutembelea katika  
**wahealthplanfinder.org**



Pakua programu ya  
**WAPlanfinder**

wahealthplanfinder.org  
1-855-WAFINDER | 1-855-923-4633

 **washington  
healthplanfinder**  
click. compare. covered.